# SHULE YA SEKONDARY YA HARRISONBURG
# KITUO CHA USHAURI

Decemba 2022

Ndugu Familia ya wanafunzi wanao ingia Darasa la 9,

Karibuni katika shule ya Sekondari ya Harrisonburg! Tuna furaha kuwa na mtoto wako HHS Blue Streak mwaka wa masomo wa 2023-2024. Tafadhali jumuika nasi kwa matukio yanayo kuja.

**Matukio muhimu kwa  Wazazi na Wanafunzi**

**Siku ya Tatu, Januari 11, 2023**

**Wanao ingia Darasa la 9. Usiku wa Taarifa kwa Familia, Ukumbi wa HHS**

**Muda:** Saa 12:00 za Jioni (watafsiri wa Lugha watakuwepo)

Chaguzi kwa njia ya mtandao utakuwepo kwa kiingereza na kispanishi: kiunga kitawekwa kwenye tovuti ya HHS

Saa 11:15 - 12:00 za Jioni kuonyeshwa maeneo ya shule

Idara ya Ushauri ya HHS itaweka matakwa ya kupata diploma, Kozi zinazotolewa, na shughuli zilizopo kwa wanafunzi kwa miaka yao ya masomo ya sekondari.

**Siku ya Nne, Januari 26, 2023**

**Usiku wa ACP - Usiku wa Mipango ya Kazi na Masomo “Academic and Career Planning” kwa wanafunzi wote wanaoingia darasa la 9, HHS**

Muda: Saa  12:00 Jioni - 2:00 Usiku

Wanafunzi na familia wanaalikwa kuhudhulia vipindi na kusikiliza na kuongea moja kwa moja na walimu na wanafunzi wa madarasa ya juu kuhusu program, madarasa, na mipango baada ya elimu ya sekondari.

Mwezi wa Pili, taarifa juu ya chaguzi za kozi zitakuwepo kwenye tovuti ya HHS kwa wanafunzi na familia. Wanafunzi watachagua kozi za darasa la 9 kwenye powerschool kuanzia mwezi wa Pili chini ya usaidizi wa washauri wa Shule za kati na wa sekondari. Kila mwanafunzi wa shule za kati watatembelea shule ya Sekondari ili kuwa na uzoefu wa HHS. Tafadhali, ongea na shule yako juu tarehe ya ziara.

Mwezi wa Tatu, Washauri wa HHS watatembelea kila shule ya Kati kuonana na mwanafunzi mmoja mmoja. Mwisho, Wanafunzi wote wa darasa la 9 wataalikwa mwezi wa nane kwenye siku ya kutembelea shule. Kawaida hii inafanyika Siku ya Nne ama ya Tano kabla ya Juma moja ya kuanza masomo.

Tafadhali wasiliana na shule kama una maswali yoyote. Taarifa zitawekwa kwenye tovuti ya HHS. Tunaangazia kukuona Januari 11!


Melissa D. Hensley, EdD — Mkuu wa Shule

Ms. Danielle Brino — Mkurugezi wa Ushauri wa Shule